# Uhuru na Amani

GAZETI LA KANISA LA KIINJILI LA KILUTHERI TANZANIA TOLEO LA 1 2017 Bei Sh. 1,000/-




## TOLEO MAALUMU

## Matengenezo: Miaka 500

ISSN 0856 - 1214

## YALIYOMO NDANI


- Juma la Matengenezo KKKT
- Maudhui ya Hoja 95 za Luther
- Matengenezo na uumbaji
- Wokovu na matendo ya sheria
- Elimu ya Kikristo ni kwa nani?
- Kuanza kwa madhehebu



MCHG.

# AMOS KAMUGISHA MUSHENDWA

(B.D, M.A in Community and Economic Development)

**Mafundisho anayotoa:**

1. Malezi, Uongozi na Maendeleo ya Vijana kwa Vijana Wakristo na Vijana kwa ujumla
2. Ujasiriamali na Maendeleo, kipekee kwa misingi ya Maandiko Matakatifu - Biblia
3. Uwakili wa Kikristo
4. Kufundisha na Kuhubiri Neno la Mungu katika semina na mikutano ya Injili

Mchg. Amos Kamugisha Mushendwa ana uzoefu katika shughuli za Uongozi na Maendeleo ya Vijana kwa miaka 31, kati ya hiyo miaka 16 katika utendaji wa moja kwa moja akifanya kazi na vijana wakiwemo wanafunzi wa sekondari, vyuo na vyuo vikuu. Ana uzoefu wa shughuli za kimataifa katika nchi zaidi ya 30 duniani. Amehudumu katika KKKT Dayosisi ya Kaskazini Magharibi: 1998 - 2005, Jumuiya ya Kikristo Tanzania (CCT): 2006 - 2013 na World Student Christian Federation (WSCF) : 2013 - 2016.

MAWASILIANO :
Simu: +255 (0) 758 031 320
+255 (0) 682 901 129
Barua Pepe: akmushendwa@gmail.com

Tangazo hili ni kwa udhamini wa:
TALANTA DEVELOPMENT CENTRE FOR PUBLIC SPEAKING
P.O. Box 6304
Dar es Salaam. Tanzania.
Simu: +255 (0) 674 348 667
Barua Pepe: info@talanta.co.tz
Tovuti: www.talanta.co.tz

Uhuru na Amani

**Uhuru na Amani**
Gazeti la KKKT
**Toleo la 1, 2017**
Na. 1 Vol. 117
**ISSN 0856 - 1214**

Uhuru na Amani ni Gazeti la Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT). Hutayarishwa na Kitengo cha Mawasiliano, KKKT.

Maoni yaliyomo katika makala zinazochapishwa ni ya mwandishi anayehusika na wala hayawakilishi mawazo ya Kanisa ama mhariri isipokuwa pale ambapo imetamkwa wazi. Ukiwa na maoni, ushauri, makala au maswali mwandikie:

**Mhariri**
**Uhuru na Amani**
**S.L.P. 3033**
**ARUSHA**
**Barua pepe:** elobulu@elct.or.tz
**Sms** Whats App kwa Mhariri:
+255-754-482-285
**Fungua Tovuti ya KKKT:**
http://www.elct.org/

**MHARIRI**
**Elizabeth Lobulu**

Limepigwa Chapa na:
**Moshi Lutheran Printing Press**
S.l.P 301 Moshi
lutheranpress@yahoo.com

Newspaper Design & Typesetting:
**Elizabeth Lobulu**

**Wachangiaji wa Makala:**
Askofu Dkt. Abednego Keshomshahara
Mch. Dkt. Emmanuel Kileo
Mch. Dkt. Faith Lugazia
Mch. Dkt. Msafiri Mbilu
Mch. Anza Amen Lema
Theol. Martha Massawe
Mch. Emeline Ndossi

**Wachangiaji Picha:**
Daniel Mwakihaba
Michael Shayo
Antje Lanzendor, Leipzig

**PICHA YA JALADA:**
**Maandamano wakati wa Ibada ya Ufunguzi wa Mkutano wa Wachungaji wote wa KKKT uliofanyika Chuo Kikuu cha Dodoma, Septemba mwaka jana.**
(PICHA: © 2016 KKKT/ DANIEL MWAKIHABA)

# MAONI YA MHARIRI

## Ukuhani ni kwa waaminio wote

Oktoba Mwaka huu 2017 Makanisa ya Kilutheri duniani yataadhimisha Kumbukumbu ya “Miaka 500 ya Matengenezo ya Kanisa”. Ni kwa kuitikia wito na kuenea duniani kote kwa Matengenezo ya Kanisa yaliyoanzishwa miaka 500 iliyopita ndiyo sababu Kanisa la Kilutheri limeenea duniani. Kuna mambo ambayo Dkt. Luther hakuona yako sawa, je hayo ni mambo gani?

Alipopigilia juu ya lango la Kanisa Kuu la Wittenberg, Ujerumani “Hoja 95” tarehe 31 Oktoba 1517 pamoja na mambo mengine, Dkt. Martin Luther aliyakataa mafundisho potofu aliposema: “Kila mkristo anayejutia dhambi zake na kutubu kweli anayo haki ya kusamehewa dhambi hata pasipo hati”.

Ungamo la Augsburg linaweka wazi kwamba Wachungaji au makasisi ni wakristo kama wenzao ila wametengwa kwa kuwekewa mikono ili kuongoza Usharika, kusimamia, kufundisha Neno la Mungu na kutoa Sakramenti.

Pia Mkristo wa kawaida hayuko chini ya kongwa la yeyote yule anayejiweka kuwa kiunganishi kati yake na Mungu.

Wapo watu wanaodhani kuna watu walio na mawasiliano ya moja kwa moja na Mungu kuliko wengine kiasi kwamba wako radhi hata kutoa fedha ili waombewe na hao “mitume-viunganishi”.

Kwa upande mwingine kuna wanaofikiri kwa kuwa ‘ukuhani ni kwa waaminio wote’; basi wao hawahitaji tena kuwa na wachungaji au daraja la uchungaji.

Fundisho la ukuhani wa waaminio wote hupinga mafundisho yasiyo ya Kibiblia yanayosisitiza Wachungaji au makasisi wanao upekee wa kitabaka kuliko waaminio wengine kwa mambo ya kiroho na kiwango cha utakatifu.

Dkt. Frederick Shoo ambaye ni Mkuu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) alitoa maelezo haya kwa ufasaha katika moja wapo ya Sura za Kitabu kipya cha KKKT kinachoitwa “Umoja na Utambulisho Wetu”.

Kutolewa kwa kitabu ni jitihada za Kanisa za kuwakumbusha viongozi wa Kanisa na washarika kwa ujumla kuhusu mambo ya msingi ya utambulisho wa wana-KKKT uliotokana na “Matengenezo ya Kanisa”. Kitabu Kitabu hiki muhimu kina mada zilizoandikwa na watu mbalimbali na kinapatikana Ofisi za Dayosisi na Ofisi Kuu ya KKKT. Pia soma makala katika toleo hili maalumu la gazeti ambalo linaelezea chimbuko la “Matengenezo ya Kanisa” na ufafanuzi wa mambo mbalimbali.

# Miaka 500 ya Matengenezo: Kanisa kuwa na kongamano

**Ili kuadhimisha vizuri tukio la Kihistoria kukumbuka "Miaka 500 ya Matengenezo ya Kanisa" (1517 - 2017) kutakuwa na matukio katika Sharika za KKKT, Dayosisi hadi ngazi ya Kanisa kitaifa. Ujumbe muhimu ni wa kuokolewa kwa 'Neema tu' kwa njia ya 'Imani katika Yesu Kristo'.**

Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) limeteua Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira (TUMA) kuwa mahali pa kuadhimisha "Miaka 500 ya Matengenezo ya Kanisa" ngazi ya kitaifa.

Katibu Mkuu wa KKKT, Bw. Brighton Killewa, alisema hayo baada ya kikao cha Kamati ya Utendaji kilichofanyika Arusha Machi 2017.

Matukio yaliyopangwa ni pamoja na kuzindua kitabu; kongamano na kuzindua mnara wa kumbukumbu. Alieleza kutakuwa na maonesho ya kazi za Vyuo vya Theolojia vya Kanisa; tamasha la uimbaji; upandaji miti na Ibada.

Wawakilishi kutoka Dayosisi zote za KKKT, maeneo ya misioni, vituo vya Kazi za Umoja KKKT watakuwepo.

Na mwaliko utatolewa kwa wawakilishi wa kiserikali, makanisa dada, makanisa mengine na vyama vya misioni.

# Maana ya rangi za Nembo ya Luther

Mwaka 1530 Martin Luther aliandika yafuatayo kuelezea maana ya rangi za ua ambalo lilikuwa nembo ya kuutambulisha Ulutheri.

Kwanza, ni msalaba mweusi uliochorwa katika moyo ulio katika rangi yake halisi. Hii ni kukumbusha kwamba imani katika Kristo aliyesulubiwa ndio inayotuokoa. Mtu ye yote aaminiye hayo toka moyoni atahesabiwa haki (Warumi 10:10). Ni msalaba mweusi unaodharauliwa na kusababisha maumivu, lakini unauacha moyo katika rangi yake ya asili. Hauharibu asili, kwa maana kwamba hautufanyi tufe bali kutupa uhai. "Mwenye haki ataishi kwa imani katika Yeye aliyesulubiwa," (Rum1:17).

Moyo upo katikati ya ua jeupe la waridi. Hii ni kuonesha kwamba imani inakupa furaha, faraja na amani - inamweka muumini katika ua jeupe la waridi lililo alama ya furaha. Imani haitoi amani na furaha kama ulimwengu utoavyo (Yn.14:27). Na ndio sababu waridi lazima liwe jeupe na siyo jekundu. Rangi hiyo nyeupe ni rangi ya roho na malaika (Mt 28:3; Yn.20:12).



Waridi lenyewe liko katika uwanja wa anga la kibuluu kuashiria roho yenye furaha; na imani ambayo ni mwanzo wa furaha ya baadaye ya mbinguni; inayoanza tangu sasa lakini hufahamika kwa matumaini, ambayo hayajawa waziwazi.

Uwanja wa kibuluu umezungukwa na pete ya dhahabu kwamba baraka za kimbingu zinadumu milele bila mwisho. Kubarikiwa kimbingu ni jambo la kupendeza upeo, zaidi ya furaha zote na bora kuliko miliki yoyote kama vile dhahabu ilivyo kito cha thamani kupita madini yote.

## Bustani zinaashiria kuenea kwa Matengenezo ya Kanisa

**Upandaji miti ni tendo kubwa linalofanyika na Walutheri kuashiria kuenea duniani kote kwa "Matengenezo ya Kanisa" yaliyoanzishwa na Martin Luther miaka 500 iliyopita.**

**Mnamo 23 Juni, 2013 Mkuu wa KKKT Awamu ya Nne, Askofu Dkt. Alex Malasusa na viongozi wengine wa Kanisa toka ndani na nje ya nchi, walipanda miti Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira walipoadhimisha miaka 50 ya KKKT.**




**Kibao cha maelezo kinasema: Mti uliopandwa na Askofu Malasusa TUMA una uhusiano na mti uliopandwa na KKKT katika 'Bustani ya Luther' iliyopo Wittenberg, Ujerumani.** (PICHA: ANTJE LANZENDORF, MISIONI YA LEIPZIG)

# Ratiba ya Juma la Matengenezo 2017

Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) limepanga matukio ya kuadhimisha "Miaka 500 ya Matengenezo ya Kanisa" kama ifuatavyo ngazi ya Dayosisi, Sharika na Vituo vyake:

**01.10.2017**
- Siku ya mwanzo ya maadhimisho ya Juma la Mategenezo ya Kanisa
- Ibada maalumu ifanyike
- Mtaalamu awepo kufundisha kusudi na historia ya Matengenezo ya Kanisa
- Tamasha la Uimbaji

**02.10.2017**
- Siku ya Vijana
- Miti ipandwe
- Kujitolea damu inapowezekana
- Kutembelea watu walio na uhitaji katika jamii

**03.10.2017**
- Siku ya Wanaume
- Wanaume na Huduma za Udiakonia
- Maombi kwa wagonjwa
- Usafi wa mazingira
- Kongamano la wanaume na wavulana

**04.10.2017**
- Siku ya Wanawake
- Wanawake na Huduma za Udiakonia
- Maombi kwa wagonjwa
- Usafi wa mazingira
- Kongamano la wanawake na wasichana

**05.10.2017**
- Siku ya Vituo vya Kanisa ngazi zote
- Vipindi vya dini mkazo uwe kuhusu matengenezo
- Watoe huduma za kijamii
- Wapate maelezo ya kusudi na historia ya matengenezo
- Utoaji damu inapowezekana

**06.10.2017**
- Siku ya Watoto
- Mchungaji aongoze Ibada ya Watoto
- Igizo
- Kwaya au nyimbo

**07.10.2017**
- Iwe ni Siku ya Watu wote
- Usafi wa mazingira
- Tamasha la uimbaji

**08.10.2017**
- Siku ya Kilele
- Ibada iwe ni moja tu inapowezekana
- Kwaya ya halaiki iimbe siku hiyo
- Tamasha la Uimbaji

# TOLEO MAALUMU: MIAKA 500 YA MATENGENEZO YA KANISA 1517 - 2017

## Wokovu siyo biashara - Mkuu



**Askofu Dkt. Fredrick Shoo, Mkuu wa KKKT.**

Mwovu hutumia mbinu ya kuwajaza watu hofu ya maisha kiasi cha kuwageuza mawindo ya watu wenye mafundisho yasiyoendana na ukweli wa Neno la Mungu, hayo yalisemwa na Mkuu wa KKKT, Askofu Dkt. Fredrick Shoo, hivi karibuni.

Akirudia aliyoyasema wakati akifunga Mkutano wa Wachugaji wote wa KKKT uliofanyika Dodoma, alisema tunapoelekea kukumbuka 'Miaka 500 ya Matengenezo ya Kanisa' kuna kila dalili ya hali iliyokuwepo kabla ya 'Matengenezo'. Alisema: "Hizi ni nyakati kama ilivyokuwa kina Johann Tetzel (1465 - 11 Agosti 1519) walivyobuni mbinu za kuwadanganya watu ili waweze kujitajirisha.

"Tunaona pia hivi sasa kuna bidhaa nyingi zinauzwa kwa jina la Yesu; na bidhaa hizi kwa masikitiko makubwa ni pamoja na wokovu ambao tunapewa kwa neema ya Mungu tu.

"Katika mambo yote tuliyojifunza katika Mkutano wa Wachungaji, naona lililo hatari sana ni hili la watu wakishajazwa hofu, wokovu nao unageuzwa kuwa biashara.

"Na hatari hii iko hata miongoni mwa baadhi ya watumishi wa Kilutheri ambao wakati mwingine wameona watumishi wametumia mbinu hizo ili kujipatia mapato makubwa, basi na sisi tunataka kuiga hivyo.

"Napenda kuwaambia kwamba utumishi wetu si kwa ajili ya kufanya biashara. Mungu ana namna nyingi za kututunza tukifanya kazi kwa uaminifu. Siyo kila mtindo tutaiga hata kama ni wa kupotosha eti kwa sababu unaleta watu wengi na kwa sababu unaleta mapato mengi. Tuwe waangalifu kwa hilo", ilisema sehemu ya hotuba yake.

Alitoa mfano wa watu kutothamini walichonacho akieleza mfano alioutoa Baba wa Taifa Mwl. Julius Nyerere kuhusu watu wapumbavu waliokuwa wanataka kuuza almasi. Na akatokea mtu mwenye vipande vya chupa za rangi mbalimbali na kuwadanganya kwamba walizonazo si almasi ila alizonazo yeye ndio almasi.

Na wale kwa kutotambua uzuri wa walichonacho, wakadharau almasi eti kwa kuwa tu mtu huyo alikuwa na makeke. Wakasema, 'si ajabu hizi tulizonayo siyo almasi' ndipo wakapokea vipande vya chupa na kubadilishana na zile almasi za kweli.

Mkuu alifafanua kwamba huenda ndio kitu kinachofanyika sasa hivi na kutahadharisha:

"Si kila king'aacho ni dhahabu. Siyo kila mtindo unaokuja sasa unafaa kuigwa. Ni matumaini yangu kwamba baada ya mkutano huu washiriki wote turejezwe kama tulivyoelekezwa katika mafundisho ya msingi ya Ulutheri wetu. Wala tusikubali kupokea wanaokuja na vitu na mitindo au mbwembwe za kila aina bila kujua uzuri au ubaya wake.

"Yule mwovu anaweza kutusahaulisha uzuri uliopo katika mafundisho yetu ya Kilutheri kuhusu Matengenezo hivyo akatudangaya na vitu vyenye matunda au matokeo ya muda mfupi ambavyo si vitu vya uzima wa milele".

**Soma Hotuba yote kutoka tovuti ya KKKT:**
www.elct.org/news/2016.11.28.Hotuba-ya-Mkuu-wa-KKKT-ya-kufunga-Mkutano-wa-Wachungaji-2016.pdf

## Wachungaji waahidi kuimarisha umoja

Wajumbe wa Mkutano wa Wachungaji toka Dayosisi, Maeneo ya Misioni na Vituo vyote vya Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), pamoja na mambo mengine, wameahidi kwa upya kutimiza wajibu wa kukuza na kulinda umoja wa Kanisa.

Washiriki hao wapatao 1,500 wamekubaliana kuombea umoja na kutoa ushirikiano katika kukusanya na kuwashilisha kwa wakati michango ya hali na mali ili kutunza kazi za pamoja.



**Wajumbe wapatao 1,500 walihudhuria Mkutano wa Wachungaji wa KKKT Septemba, 2016.** (PICHA: © 2016 KKKT).

# Ibada ni utambulisho muhimu wa wana-KKKT

Mchg. Dkt. Msafiri Mbilu

Wataalamu wa mambo ya dini wanasema: “Kwa ujumla dini zote zinafanana kwa kuwa kila dini ina kusudi la kumwabudu Mungu wake, tofauti kubwa inayozifanya dini ziwe tofauti ni mtindo wa Ibada.”

Wakristo wana madhehebu mbalimbali na kinachowatofautisha ni ile namna ya kumwabudu Mungu.

Siku hizi kutokana na shida kubwa ya ajira, kazi ya Uchungaji imeingiliwa sana. Baadhi ya watu wanadhani wanaweza kujiita wachungaji bila mafundisho yoyote.

Wapo baadhi ya Wachungaji wa Kilutheri katika nyakati hizi wameanza kudharau utambulisho wao katika ibada. Wamechotwa na vikundi vilivyoko huko mtaani na kuona kuwa labda ibada zao zinafaa zaidi. Kanisa liweke utaratibu wa kufuatilia ili kuhakikisha kuwa Ibada zetu zinafanana na kufuatwa ipasavyo.

Kilele cha ibada ya Kilutheri ni Mimbarani ambapo Neno la Mungu linahubiriwa kwa usahihi wake. Martin Luther akikaza kuwa ni katika Neno likihubiriwa kwa usahihi wake ndipo watu watatambua kwamba wokovu wao unaopatikana kwa imani.

Hivyo kipindi cha mahubiri kipewe muda wa kutosha katika ibada zetu. Katika ibada nyingi siku hizi matangazo yamepewa muda mrefu zaidi kuliko mahubiri.

**Soma Mada yote kutoka tovuti ya KKKT:** www.elct.org/documents/2016.11.Mada-kuhusu-Umoja-wa-Kanisa.pdf



Ibada ni njia moja inayoweka utambulisho wetu kwa wazi sana.
(PICHA: © 2016 KKKT/ DANIEL MWAKIHABA).




Mchg. Dkt. Msafiri Mbilu, Mkurugenzi Chuo Kikuu cha Sebastian Kolowa, Tawi la Tanga.



Wakristo wakihubiriwa Neno kwa usahihi wake ndipo watakapotambua wokovu wao unaopatikana kwa imani.



# Wabadilishana ofisi kwa amani

Moja ya sifa za Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) ni pamoja na utaratibu lililojiwekea wa kuchagua viongozi wake kwa amani. Hivi karibuni Mkuu wa KKKT Awamu ya Nne Askofu Dkt. Alex Malasusa alikabidhi rasmi majukumu ya Ofisi kwa Mkuu wa Tano wa KKKT Askofu Dkt. Fredrick Shoo.



Kutoka kulia: Katibu Mkuu wa KKKT, Bw. Brighton Killewa; Askofu Dkt. Solomon Massangwa wa Dayosisi ya Kaskazini Kati, Mkuu wa KKKT, Askofu Dkt. Fredrick Shoo; Mkuu wa KKKT Awamu ya Nne, Askofu Dkt. Alex Malasusa, Mwenyekiti Halmashauri ya Wanawake KKKT, Bibi Mary Laiser na Mwenyekiti Halmashauri ya Fedha, CPA Yona Killagane. (PICHA: © 2017 KKKT/ E. LOBULU).

# Hakuna anayeokolewa kwa matendo ya sheria

Na Askofu Dkt. Abednego Keshomshahara

Matengenezo ya Kanisa yanatukumbusha kuwa mwanadamu hawezi kuokolewa kwa njia ya matendo ya sheria.

Mafundisho rasmi ya Kilutheri yanasema tunapokelewa jinsi tulivyo lakini hatupaswi kubaki jinsi tulivyopokelewa. Inatupasa kuendelea kubadilishwa hadi pale tutakapomwona Mungu uso kwa uso. Na hatua ya kubadilishwa ni ya utakaso. Mtume Paulo anasema katika Rum 6:1-4 kuwa tunapookolewa kwa neema hatupaswi kuishi katika dhambi bali inabidi tubadilike na kuwa na maisha mapya. Kwa sababu hii, anazidi kusema "ya kale yamepita tazama yamekuwa mapya" (1Kor. 5: 17).

Kwa miaka mingi tumekazia neema tukasahau utakaso ambapo inabidi imani izae matunda ya imani ambayo yanathibitisha kuokolewa kwetu.

Katika Mt 7:19 Neno linasema "mti usiozaa matunda utakatwa." Na katika Mt 25: 36 - 46 tunaambiwa kuwa siku ya mwisho kigezo cha kurithi uzima au kutorithi uzima ni jinsi tulivyojali na kutendea wengine: kuwavika nguo walio uchi, kuwalisha wenye njaa, kutembelea wagonjwa, walio kifungoni,



Askofu Dkt. Abednego Keshomshahara, KKKT Dayosisi ya Kaskazini Magharibi.

nk.

Utakaso ni kazi ya Roho Mtakatifu inayotutaka tutubu dhambi, tusamehe dhambi, tuwe na upendo, tujitoe na kutoa mali zetu kwa ajili ya kazi ya Mungu, kumtumikia Bwana, kuomba Mungu na kuzaa matunda ya imani.

Mwanzilishi wa matengenezo ya Kanisa Dkt. Martin Luther alisimamia ukweli wa Neno la Mungu katika kupambana na mafundisho potofu yaliyofanya wokovu ufikie hatua ya kununuliwa kwa hela kupitia vyeti vya msamaha.

Dkt. Luther alisisitiza kwamba Matengenezo ni jambo linaloendelea siku kwa siku; kizazi hadi kizazi.

## Matokeo

Mageuzi na mabadiliko yaliyoletwa na Matengenezo ya Kanisa yaligusa mitazamo ya kidini kiasi kwamba mabadiliko yaligusa si tu Kanisa la Kirumi bali pia wanamatengenezo wenyewe walifikia hatua ya kutopatana.

Walitofautiana kiasi cha kuwa na madhehebu mbalimbali kwa sababu walikuwa na mitazamo tofauti ya Kibiblia na kitheologia. **--Askofu Dkt. Keshomshahara**

**Jisomee mada hii kikamilifu toka tovuti ya Kanisa: www.elct.org/documents/2016.11.Mada-kuhusu-Miaka-500-ya-Matengenezo.pdf**



**Baadhi ya viongozi wa KKKT wakiwa na Waziri wa Mambo ya Ndani, Mhe. Mwigulu Nchemba, aliyefika UDOM kuusalimu Mkutano wa Wachungaji wa KKKT Septemba 2016 ambapo aliwasilisha mchango wake wa hiari.**

# KKKT ni tunda la matengenezo

Matengenezo yametokeza sura ya wakristo duniani kuwa na Makanisa ya Kilutheri 145 wanachama wa Fungamano la Makanisa ya Kilutheri Duniani likiwemo Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT).

Makanisa haya yana wakristo zaidi ya milioni 70 katika nchi 79. Yapo Makanisa ya "reformed" yanayofuata mafundisho ya John Calvin na "Muungano wa Walutheri na "reformed" yenye makanisa 227 na wakristo milioni 80 kwenze nchi 108, na hivyo jumla ya makanisa ya kimatengenezo, yaani walutheri na "reformed" ni zaidi ya washarika milioni 150.

Haya ni matokeo ya matengenezo yaliyoanzishwa na Martin Luther (Ujerumani), John Calvin na Huldrych Zwingli (Uswizi) ambapo baadaye makanisa haya yalisambaa duniani kote.

Takwimu zinaonesha kuwa makanisa ya matengenezo, makanisa ya kipentekoste na kikarizimatiki yana takribani wakristo bilioni moja ambapo wakatoliki ni bilioni 1.2 hivyo kuwa na jumla ya wakristo bilioni 2.2 duniani. Kanisa la kwanza kwa ukubwa FMKD ni Kanisa la Kiinjili Makane Yesu la Ethiopia likifuatiwa na KKKT.

# Fungamano la Makanisa ya Kilutheri Duniani

Mkutano Mkuu wa 10 wa Fungamano la Makanisa ya Kilitheri Duniani (FMKD) utafanyika 10 - 16 Mei, 2017 Windhoek, Namibia. Mada Kuu: 'Nimekombolewa kwa Neema ya Mungu'. Mada ndogo chini ya Neno kuu ni: Wokovu si wa Kuunza; Binadamu si wa Kuuzwa na Uumbaji si wa Kuuzwa".



**Viongozi wa Makanisa, Wachungaji na washiriki wengine waliokutana Moshi mwaka 2015 kuadhimisha miaka 60 ya Mkutano wa Marangu kama sehemu ya maandalizi ya mkutano wa 12 wa FMKD.** (PICHA: © 2015 KKKT).

# Martin Luther ni nani



Dkt. Martin Luther.

**MAHALI ALIPOZALIWA**

Dkt. Martin Luther alizaliwa mjini Eisleben, Ujerumani 10 Novemba 1483. Kesho yake ilikuwa siku ya Mtakatifu Martinus hivyo alibatizwa katika Kanisa la Mtakatifu Petro Paulo, akaitwa Martinus kwa Kilatini yaani Martin.

**HALI YA MAISHA YA WAZAZI**

Wazazi wake walikuwa ni Hans na Margarette Luther. Mzee Hans alikuwa ni mtoto wa mkulima ambaye aliamua kutoka Thueringia na kwenda Eisleben kutafuta maisha na baadaye alihamia Mansfeld mwaka 1484. Huko alifanikiwa kumiliki kiwanda cha kutengeneza vifaa vya shaba japo alinunua kiwanda hicho kwa mkopo aliopaswa kuulipa maisha yake yote.

Martin Luther alipelekwa shule Mansfeld ambapo alisoma kwa miaka tisa mfululizo bila likizo. Alipotimiza miaka 14 alipelekwa Shule ya Magdeburg na kisha alipelekwa kusoma Eisenach mji ambao mama yake alizaliwa.

Baba yake aliamua Martin aende kusoma sheria kwenye Chuo Kikuu cha Erfurt akiwa na umri wa miaka 17 ili baadaye aje awasaidie wazazi wake wakizeeka. Katika Chuo Kikuu cha Erfurt, Martin Luther alisoma sheria shahada ya kwanza na ya pili. Akiwa Erfurt ndipo aliona Biblia kwa mara ya kwanza kwenye maktaba ya chuo.

**AHADI YA KUWA MTAWA**

Akiwa anasoma Sheria tarehe 2 Julai 1505 aliwatembelea wazazi wake mjini Mansfeld na wakati anarudi ilinyesha mvua kubwa ya radi iliyomtisha kiasi cha kutoa nadhiri akisema: "Mtakatifu Anna, niponye na radi hii, nikipona naahidi kuwa mmonaki" au mtawa. Mtakatifu Anna, aliheshimiwa kwa wakati huo kwa kuwa na wajibu wa kulinda wachimba madini ya shaba na wahunzi wa vifaa vya shaba. Mtakatifu Anna ni mama wa Bikira Mariamu. Baba yake Martin Luther aliumizwa kwa kupoteza matumaini ya kutunzwa na mtoto wao uzeeni. Martin aliwaambia wazazi wake kuwa angewasaidia kwa maombi zaidi ya ambavyo angewasaidia akiwa mwanasheria.

Kwa kuwa Mzee Hans alimwamini Mungu sana, alipokea hali ya mwanawe kuwa mmonaki. Hans Luther alijua wokovu ni kitu muhimu katika maisha. Martin Luther alichagua kuwa mmonaki katika Shirika la Mtakatifu Augustino lililokuwa karibu na Chuo Kikuu cha Erfurt.

**AWA PROFESA NA KASISI**

Luther alihamia Wittenberg mwaka 1511. Baadaye alichukua masomo ya Udaktari wa Theologia na akawa mhubiri kwenye Kanisa la Ikulu ya Mfalme. Alikuwa padre wa Kanisa Katoliki 1507 hadi alipokuwa na miaka 40.

**AHADI YA KUKEMEA UONGO**

Kama Profesa wa Chuo Kikuu alikuwa ameapa kusema ukweli na kukemea uongo.

**FAMILIA NA KIFO**

Akiwa na miaka 41 Martin Luther alioana na Catherine von Bora (26) na walijaliwa watoto sita. Alifariki 1546.

## Matokeo chanya ya Matengenezo

Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania limeenea mikoa yote likiwajali watu kwa kutoa huduma za kiroho na kimwili kwa upendo bila ubaguzi wa kieneo, kabila, taifa au mipaka.

## LENGO LA LUTHER

**Mnamo 31 Oktoba 1517 Dkt. Martin Luther alibandika hoja 95 dhidi ya uuzaji wa vyeti vya msamaha. Hoja hizo ziliandikwa kwa lugha ya Kilatini na hakuwa amefikiria mapinduzi makubwa ndani ya kanisa bali alipenda kulisaidia pamoja na mambo mengine, ili Kanisa liache utaratibu wa kuuza vyeti vya msamaha wa dhambi.**

# HOJA 95 ZA LUTHER

**UTANGULIZI**

Kwa hoja alizotoa Martin Luther lengo lake kwa kifupi alitaka matengenezo au mabadiliko katika mambo matatu:

Kanisa lisiendelee kuuza hati za msamaha wa dhambi zilizouzwa ili kupata fedha kwa ajili ya ujenzi wa Kanisa la Rumi (St. Peter's Basilica). Aliona kwamba msamaha ni jambo binafsi kati ya mtu na Mungu wake na kwamba huwezi kusamehewa dhambi kwa kuwa tu umenunua cheti. Mungu humsamehe anayetubu kwa kuwa Yeye ni mwenye huruma.

**IMANI KWA KRISTO PEKEE**

Pili alisisitiza imani kwa Yesu Kristo peke yake ndiyo iliyo muhimu katika wokovu.

**NENO TU NDIO CHANZO CHA KWELI**

Tatu alisisitiza kuwa Neno la Mungu ndio chanzo cha ukweli kuhusu maisha ya ufuasi kwa viongozi wa Kanisa na waumini. Hivyo akashauri kila mtu ajisomee Neno la Mungu au Biblia kila siku maana kila siku mtu husahau kile alichosoma na si lazima asomewe na kiongozi wa dini. Aliamua kutafsiri Biblia toka Kilatini hadi Kijerumani na ndio ulikuwa mwanzo wa Biblia kutafsiriwa kwa lugha mbalimbali duniani. Katika tafsiri hiyo ndipo baadhi ya vitabu vya apokrifa viliondolewa. Kuanzia hapo watu wakaanzisha vikundi vya kujifunza Biblia (Bible Study) na matengenezo yakaenea duniani.

**TUNAHESABIWA HAKI KWA IMANI TU**

Luther 'alifunguliwa' baada ya kusoma Waraka wa Paulo: ***"Mwenye haki ataishi kwa imani"*** (Rum 1: 17). Alitafakari na kugundua kwamba wenye haki watafika mbinguni kwa imani pekee na siyo kwa matendo mema. Kwa maneno mengine ni kwamba neema ya Mungu ni kitu kinachotolewa bure kwa wanadamu na hatukipati kwa uwezo wetu. Alikataa mafundisho kwamba imani lazima iambatane na matendo mema ili kupata wokovu.

**WOKOVU NI KWA NEEMA TU**

Aliamini kwamba matendo ya mtu hayakuwa na ushawishi wowote kwa Mungu na kwamba wokovu ni kwa njia ya neema tu. Mungu huwapa waaminio wokovu kwa kuwa ni mwenye huruma.

Matengenezo yalileta kuundwa kwa Kanisa la Kilutheri duniani na mabadiliko mbalimbali yalitokea katika Kanisa na jamii kwa jumla.

# Matengenezo na wanawake

Na Mchg. Dkt. Faith Lugazia

**UTANGULIZI**

Wakati wa "Matengenezo ya Kanisa" ya Karne ya 16 huko Ulaya, mwanamke hakushirikishwa katika majadiliano na malumbano kuhusu matengenezo. Mfumo dume uliokuwa umezingira maeneo ya Ulaya ya matengenezo ni moja ya sababu zilizozuia ushirikishwaji wa mwanamke.

Kwa mfano ingawa mwana matengenezo mkuu, Martin Luther, alimpenda sana mke wake, Katharina Von Bora na kumheshimu sana, hatusikii popote anapo mhusisha ama hata kumshirikisha maandiko yake kuhusu maono yake juu ya matengenezo. Luther alimwita Katharina: "Nyota ya asubuhi ya Wittenberg" si kwa sababu aliona maono kwake kuhusu "Matengenezo ya Kanisa" bali alimuona kuwa mchapakazi za ndani na mtunzaji mwema wa familia. Kwa huduma hizo, hakika Luther alimheshimu Katharina.

Kwa habari za wanawake kushiriki katika huduma za uongozi, hasa uchungaji, Luther alitumia Mwa 3:36, 1Tim 3:2, Tito 1:6 na 1Kor 14:34 na kusema kuwa wanawake ni viumbe dhaifu, hawawezi kuhimili ushindani kwa huduma ya kichungaji na kwa sababu hiyo hata alishauri wasifikiri ama kupendelea kuingia katika huduma ya uchungaji. Mafundisho haya yanapatikana katika andiko lake: "Martin Luther, On the Councils and the Church 1539" (nukuu kutoka LW 41, 148-156.164-167). Hata hivyo, kuna mafundisho mawili aliyohakiki ambayo ninadiriki kukiri kuwa ndiyo yamekuwa chimbuko na mlango kwa wanawake kushiriki katika matengenezo ya Kanisa leo.

**FUNDISHO LA KWANZA**

Fundisho la kwanza ni: "Ukuhani ni kwa wote waaminio." Alieleza kuwa baada ya kubatizwa, kila muumini anayo nafasi na haki ya kumshuhudia Kristo kwa wengine na hata kushiriki haki na wajibu wowote ndani ya Kanisa. Andiko lake lilitokana na malumbano kati yake na uongozi wa Kirumi Katoliki waliokuwa wakijiwekea tabaka kwamba viongozi wa kiroho wanahitaji kupatiwa nafasi za pekee na hata kutotozwa kodi kwa kuwa wao ndiyo wawakilishi wa Mungu duniani. Luther alisema hapana, kwa habari ya Ukristo na ushuhuda wa Kristo, sote wanawake na wanaume ni makuhani.

**FUNDISHO LA PILI**

Alitoa fundisho lingine kuwa "Kanisa lililokubali kutengenezwa (kukosolewa) linahitaji kujitengeneza kila mara."

Alipogundua kuwa pamoja na mengi aliyoyasema ili yasaidie kutengeneza Kanisa bado kulikuwa kuna mengi ya kurekebisha na kwa hiyo kutengeneza Kanisa, jambo hili lisiwe la mara moja bali kwa wakati wote.

Mafundisho haya mawili yalisaidia kulitoa Kanisa katika mfumo dume na kuelekeza wazi kuwa, kumbe hata mwanamke naye anapashwa kushiriki katika huduma za kumtangaza Kristo ndani ya Kanisa.

Lakini pia maandiko hayo yakatoa mwanya kwa Kanisa (lililokuwa likiongozwa na wanaume tu) kujikosoa kuwa, kwa vile wanaume na wanawake ni wana Kanisa basi ili kukamilisha ujumbe wake wa kinabii, kikuhani na kidiakonia ni budi waumini wa jinsi zote washiriki. Ushiriki wao si habari ya haki na usawa tu kama vidaivyo vyama vya kijamii bali ni kukamilisha wito wa Mungu wa kutiisha nchi na kuleta amani kwa uumbaji wote wa Mungu (Mwa 1: 28b). Katika mchakato wa kuweka mafundisho hayo katika matendo, wanawake wakashiriki katika "Matengenezo ya Kanisa".

Wanawake hapa Tanzania hasa ndani ya Kanisa la Kilutheri waliingia wakati uleule Injili inaanza, hata kabla ya Kanisa letu kuunganika mwaka 1963.

Kumekuwa na ongezeko la wanawake wamisionari kote nchini. Tunaambiwa mwanamke kutoka kule Bukoba, Bibi Rebecca Buhimbazi, atakumbukwa kwa kazi ya kuchapa Injili katika kundi la kwanza la wahubiri, mwishoni mwa Karne ya 19. Baada ya Azimio la Arusha 1967, lililotuelekeza kujitegemaa si tu katika Serikali bali hata Kanisa wanawake wameingia sana katika kushiriki Matengenezo ya Kanisa kwa kutumia vipawa na karama yao. Si hayo tu, bali pia wanawake wamekuwa mstari wa mbele kutoa mali na muda wao kwa ajili ya Kanisa. **Mch. Dkt. Faith K. Lugazia anatoka KKKT Dayosisi ya Kaskazini Magharibi na anafanya kazi ya Umisionari nchini Rwanda.**

# Neema hutupa kuhesabiwa haki


**Ifuatayo ni sehemu ya hotuba ya Papa Francis katika Ibada maalumu iliyoandaliwa na madhehebu ya Kilutheri na Katoliki katika Kanisa Kuu la Kilutheri Lund, Sweden Siku ya Matengenezo 31 Oktoba 2016:**

**"**Wakatoliki na Walutheri tumeanza safari ya upatanisho kwa pamoja. Ujio wa maadhimisho ya Matengenezo ya Kanisa ya mwaka 1517, unatupata fursa mpya ya kupatana ili tufuatane njiani pamoja. Majadiliano ya miaka 50 baina ya Fungamano ya Makanisa ya Kilutheri Duniani (FMKD) na Kanisa Katoliki yanaonesha njia hiyo ikianza kueleweka. Hatukati tamaa kwa ufa uliotokana na tofauti za utengano wetu. Tuna fursa ya kurekebisha kilichotokea katika historia kwa kuto-endeleza malumbano ya kufarakana; mambo ambayo yanazuia maelewano.

"Tumwombe Bwana ili Neno lake lituunganishe, kwani ni chanzo cha malisho na maisha yetu; bila kuhuishwa nalo hatuwezi jambo lolote.

"Uzoefu wa maisha ya kiroho ya Martin Luther unatoa changamoto kwetu kukumbuka kwamba bila Mungu hatuwezi kufanya jambo lolote. "Nitawezaje kupokea neema ya Mungu?" Ni swali lililomkosesha amani Luther. Ni kweli suala la uhusiano binafsi na Mungu ni la msingi katika maisha.

"Kama tujuavyo, Luther alikutana na Mungu mwenye neema katika *'Habari Njema'* ya Yesu aliyetwaa mwili, akafa na kufufuka. Kwa kutumia dhana "kwa neema tu", Luther anatukumbusha kwamba muda wote Mungu ndiye huchukua hatua kwanza, kabla hata mwanadamu hajawa na itikio lolote, hata pale anapojaribu kuhuisha moyo ili kuitikia wito. Imani katika kuhesabiwa haki huelezea kiini cha uwepo wa mwanadamu mbele ya Mungu. Yesu anatuombea sisi kama mpatanishi mbele ya Baba, akiomba kwamba wafuasi wake wawe na umoja ***"ili ulimwengu upate kuamini"*** (Yn 17:21). Hili ndilo linalotufariji na kutuhimiza tuwe wamoja na Yesu, na kutufanya tuombe: 'Tupe zawadi ya umoja, ili ulimwengu uamini katika nguvu ya msamaha wako'. Huo ni ushuhuda ambao dunia inatarajia kuuona kutoka kwetu.**"**



**Kutoka kushoto: Rais wa FMKD, Askofu Dkt. Munib Younan, Papa Francis na Katibu Mkuu wa FMKD, Mchg. Dkt. Martin Junge.**

# Upotoshaji kuhusu Uamsho

Wenzetu wakiugua, mara zote hujiuliza: "Hivi shida hii imesababishwa na nini?" Na sisi Waafrika swali letu wakati wa shida huwa: "Hivi shida hii imesababishwa na nani?"

Hivyo kabla ya maombezi hasa kwa wagonjwa, na wenye shida mbalimbali ndani ya jamii mfano: kukosa mtoto, kufiwa mara kwa mara, kukosa mchumba ama kuachwa na wachumba mara kwa mara, watoto kufeli katika masomo na magonjwa kama UKIMWI, ama ya kichwa kama kichaa, ama kifafa; tumezoea kuona wana maono hufunga na kuomba kuuliza shida ya muumini imesababishwa na nani? Na hatimaye waonaji hao husema wameona aliyesababisha shida. Kundi hili ni hatari sana, kwani kwa kutumia mbinu hiyo ya mtazamo wa Kiafrika, ndugu zetu wengi wanaamini sana mambo kama hayo. Mara nyingi ataambiwa mbaya ni jamaa au ndugu wa karibu na mwenye shida. Katika hili, makundi ya uamsho wa kikarismatiki ndani ya Kanisa letu yamejikuta katika matatizo makubwa ya kimahusiano ndani ya familia.

Mafundisho ya jinsi hii, badala ya kumuonyesha Yesu wa upendo na upatanisho, yamemuonyesha Yesu kuwa ni mleta uadui.

Hivyo unakuta ndugu wameokoka na wote wako katika kundi la maombi ila hawasalimiani na hawana ushirika wa pamoja kwa madai ya kutendeana maovu.

Kuhusu karama ni Roho Mtakatifu anayetoa karama. Lakini upotofu unakuja pale: Kwanza, wanapopunguza karama za Roho Mtakatifu na kutaja nne tu. Roho Mtakatifu anapokuja kwetu kama zawadi hutoa karama mbalimbali kwetu. Ukisoma 1Kor 12-14; Rum 12:6-8; Efe 4:11 na 1Pet 4:9-11 vifungu hivi vinazungumza juu ya karama atoazo Roho Mtakatifu. Karama za Roho Mtakatifu ni Yeye Roho atoaye si Kanisa wala mtu fulani hivyo basi, ni muhimu sana tumuombe huyu Roho Mtakatifu badala ya kutafuta njia ya mkato kwa kuiga watu wengine.

Shida ya Pili, ni pale karama za Roho Mtakatifu zinapowekwa katika makundi ya karama 'kubwa na ndogo' na kudhani wenye hizo karama ndiyo wako karibu na Yesu kuliko wengine.

Shida ya Tatu, ni pale wanapotumia karama za Roho Mtakatifu kwa kujijenga badala ya kulijenga Kanisa. Wengi wenye karama za uponyaji, hujitahidi sana kuonyesha kazi yao ili wawapate waumini. Pia wenye tatizo hufikiri kuwa mwombaji ndiye yuko karibu na Yesu na hivyo humng'ang'ania huyo. Baada ya muda akijitokeza mwingine, watu wanahama, nk. Nne, pale wanapofanya watu waamini kwamba wanaweza kuwapatia karama yoyote kwa kuwaombea.

Mafundisho ya uamsho wa vikundi vya kikarismatiki vilivyomo ndani ya Kanisa yanaleta changamoto kwenye muundo mzima wa kanisa letu. Changamoto zinazosababishwa na watu kuiga mafundisho pasipo kufahamu kwa kina (copy and paste). Katika matengenezo mkazo ni kuhakikisha mtu anapata wokovu kupitia Kristo na matunda kutokana na karama za Roho Mtakatifu ni za muda mfupi. Tunapoomba Kristo ndiye mpaji na mponyaji wetu.

**Soma Hotuba yote kutoka tovuti ya KKKT: www.elct.org/documents/2016.11.Mada-kuhusu-Kanisa-na-Uamsho.pdf**



**Mchg. Dkt. Faith Lugazia,**
**Mhadhiri na Makamu Mkuu wa Kitivo cha Theolojia Chuo Kikuu cha Kiprotestanti, Rwanda.**

## Tuwe na vituo vya maombezi

Wakati umefika ambapo Kanisa letu kwa ukubwa wake linahitaji kuwa na vituo vya kuwajenga na kuwaganga watu waliovunjika moyo. Na wale ndugu zetu Wachungaji wenye karama za kikarismatiki tuwape kazi maalumu ya kuhudumu ndani ya vituo hivyo (to act as referral spiritual healing centres). **--Mchg. Dkt. Faith K. Lugazia**



(PICHA: © 2016 KKKT/ DANIEL MWAKIHABA).

## Utambulisho wa Mlutheri

*Mchg. Dkt. Angela Olotu*

Martin Luther anasema Kanisa, ni pale ambapo Injili inahubiriwa na kupokelewa na tena Sakramenti ya Ubatizo na Ushirika wa Meza ya Bwana vinatolewa kwa usahihi wake.

Mlutheri anamwamini Yesu Kristo kuwa Bwana na Mwokozi wa maisha yake na kubatizwa katika Utatu Mtakatifu, ambapo anasafishwa dhambi zake na kupokelewa katika kundi la waaminio na kufanyika mwana wa Mungu.

Mlutheri anaamini juu ya mafundisho, mafunuo, mapenzi na ahadi za Mungu kupitia Maandiko Matakatifu yaani Biblia, kuwa ndiyo msingi wa maisha yake.

Mlutheri anakubali na kuamini ya kuwa Katekisimo Ndogo ya Dkt. Martin Luther, ukiri wa Nikea, Mitume, Athanasio na Ungamo la Augusburg lisilobadilika ndio maelezo sahihi tena ya wazi ya Neno la Mungu.

Siku ya kuabudu kwa Mlutheri ni Jumapili; siku Bwana wa Kanisa, Yesu Kristo, alifufuka akiashiria ushindi na ukuu alionao juu ya nguvu ya dhambi na ya mauti (Mt 28:1; Mk 16:2 na Yn 20:1). **Mchg. Dkt. Angela Olotu ni Mkuu wa Kitivo cha Theolojia, Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira.**

# Elimu ya Kikristo ni taaluma

**Na Mchg. Dkt. Emmanuel Kileo**

Mafundisho ya kikristo kama wajibu wa Wachungaji ni hatua moja, lakini mafundisho sahihi, yanayofundishwa kwa utaratibu na weledi ni jambo la pili.

Hii ni kusema, Elimu ya Kikristo ni taaluma hivyo inatakiwa ifundishwe kwa weledi mkubwa. Na wakati wa kujibu maswali yanyoulizwa na washarika jambo hili lifanyike baada ya kutafakari kwa umakini sana. Kila mtu ana maswali mengi magumu hivyo majibu yasitolewe kwa urahisi.

Haitoshi kuwatisha wakristo kwa mambo magumu kwa kusema: "hiyo ni dhambi" au "Biblia imekataza" bila kufafanua na kudhani somo limeeleweka. Huwezi kuulizwa kwa nini tunabatiza ujibu kwa kusema "usipobatizwa ni dhambi". Kujibu hivyo ni kutokana na uvivu. Ni lazima uweze kueleza na kufafanua.

Changamoto za kimazingira na utandawazi zinafanya kazi ya Elimu ya Kikristo isimamiwe zaidi na wachungaji, tena wafanyao kazi kwa weledi na sio kuwaachia walei, wainjilisti na watu wa kujitolea usharikani.

Mafunzo kwa wachungaji yanapaswa kuwa endelevu hata baada ya kuhitimu na kubarikiwa kuwa wachungaji ili kuweza kuwafundisha na kuwasaidia washarika. Upo upotoshaji wa kila aina nje ya mfumo wa Kanisa letu kiasi kwamba kujiendeleza kielimu kutasaidia wachungaji katika kazi zao. Kuna upotoshaji wa baadhi ya wahubiri wa kuwatia watu hofu kuhusu nguvu za shetani ili wawatoe mapepo baada ya kutoa zaka au sadaka maalumu. Hata baadhi ya kwaya zimeingia katika mtego wa kutunga nyimbo za kumwinua shetani badala ya kuimba nyimbo za Injili. Miongoni mwa baadhi ya wachungaji kuna mafundisho ya kuhamasisha utoaji wa zaka ambazo hutumika kwa manufaa yao binafsi.

**Soma mada hii kwa ukamilifu kutoka tovuti ya KKKT: www.elct.org/documents/2016.11.Mchungaji-na-Elimu-ya-Kikristo.pdf**





**Mchg. Dkt. Emmanuel Kileo, Mhadhiri Chuo Kikuu Kishiriki cha Kumbukumbu ya Stefano Moshi.**




**Wakati akihubiri katika Ibada ya Kufunga Mkutano wa Wachungaji KKKT, Askofu Dkt. Emmanuel Makala, alisisitiza kwamba mafunzo ya Wachungaji yawe endelevu ili kuwasaidia washarika.** (PICHA: © 2016 KKKT).

# Elimu ya Kikristo itolewe kwa marika gani?

Elimu ya Kikristo inatakiwa itolewe kwa watu wa marika yote na kila rika kwa namna yake.

Kazi ya kufundisha Elimu ya Kikristo inamhusu Mchungaji. Yeye ni:

- Mtheologia mkuu wa Usharika
- Msimamizi wa mafundisho yote ya Kikristo Usharikani kwake.
- Msimamizi wa missioni -wito mkuu: "Enendeni ulimwenguni kote..."
- Mchungaji ni mfundishaji,
- Mchungaji ni muwezeshaji,
- Mchungaji ni mtoa dira,
- Mchungaji ni mwandaaji, nk.

# Wamisionari wa DanMission waagwa

Ofisi Kuu ya KKKT 20 Machi 2017 iliandaa hafla fupi ya kuagana na Mwakilishi wa DanMission nchini, Bw. Simon Christensen na mkewe Bibi Mette Christensen.

Wamisionari hao wamefanya kazi nchini kwa miaka mitatu na nusu: Simon akiwa mwakilishi wa DanMission na Mette ambaye ni Muuguzi alifanya kazi katika Kurugenzi ya Afya KKKT.

NKM KKKT, Mchg. Lazaro Rohho alitoa nasaha za kuwaaga wageni hao.



**Mchg. Lazaro Rohho akiongea wakati wa hafla ya kuwaaga wamisionari wa DanMission. Kutoka kulia ni Mwakilishi wa Kanisa la Kiinjili la Marekani, Mchg. Deborah Troester; Bibi Mette na Bw. Simon S. Christensen wa DanMission; na Naibu Katibu Mkuu Huduma za Jamii na Kazi za Wanawake KKKT, Mchg. Rachel Axwesso.**

# Matengenezo ya Kanisa na watoto

**Na Mtheol. Martha Massawe**

**Utangulizi**

Matengenezo ya Kanisa ni kurekebisha na kutengeneza mafundisho ya Kanisa ili liweze kufanya kazi yake ya msingi ambayo ni ujumbe wa kuokolewa kwa Neema tu kwa njia ya Imani katika Yesu Kristo. Matengenezo ya Kanisa yanatukumbusha kuwa mwanadamu hawezi kuokolewa kwa njia ya matendo ya sheria.

**Mtazamo wa Agano la kale na Watoto**

Binti Farao akamwambia, Mchukue mtoto huyu, ukaninyonyeshee, nami nitakupa mshahara wako" (Kutoka 2:9). Huyu ijapokuwa si mkristo anatufundisha wajibu wetu kama wazazi. Mtoto ni mali ya Mungu (Ezekiel 18:4).

**Hali ya Kanisa na Watoto Wakati wa Matengenezo**

Kwa wakati huo mapadri na viongozi wa Kanisa kwa ngazi zote walikuwa wamepungua uchaji na kushuka kwa maadili yao ya kazi na kwa njia hiyo kukosa ushuhuda wa Kikristo. Hali hii iliathiri watoto ndipo Wanauamsho kama John Wycliffe, Jan Huss na Martin Luther wakiwa na mzigo na maono waliona umuhimu kufanya Matengenezo ya Kanisa. Hata hivyo watoto pia walikuwa washiriki kwani hata wanauamsho hao walikuwa watu wenye watoto. Waliona upo umuhimu wa kufundisha watoto kama Yesu alivyosema "…waache watoto waje kwangu…." Hivyo ni jambo la muhimu kuwafundisha watoto kumjua Bwana wetu Yesu Kristo na kuokoka (Mit 22:6) kwa maana Mungu anawajua tangu hawajazaliwa. "Kabla sijakuumba katika tumbo nalikujua, na kabla hujatoka tumboni nalikutakasa," (Yer 1:5a). Martin Luther naye katika Katekisimo ndogo alikaza kuwafundisha watoto.



**Mtheol. Martha Massawe**

**Watoto katika Kanisa la Leo**

Kanisa lina maandiko mengi ya kufundisha watoto yakiwemo yale ya Shule ya Jumapili, Kipaimara nk., yanayoweza kuwasaidia watoto. Pamoja na hayo ufundishaji wenyewe haupewi kibaumbele ndani ya familia na kanisani kwa ujumla. Watu wengi wametunga vitabu vyao vizuri vya kufundishia watoto lakini wao wenyewe na wazazi wote, viongozi wa makanisa yaani wa maaskofu, wachungaji na wainjilisti hawatilii maanani suala la kufundisha watoto. Kwa hiyo makanisa yetu yanadhoofika na hata kufa.

Kuna miji mingi duniani hasa Ulaya makanisa yamebaki tu kuwa sehemu ya historia. Hata kwetu ni hivyo kwamba watoto anapewa kipaimara kama sehemu ya utamaduni wa mahali, utakuwaje hujabarikiwa wakati watu wote wamebarikiwa? Kipaimara inafananishwa na jando kama ilivyo katika makabila mengi ya kwetu. Au wanafundishwa ukristo au elimu ya dini ili wasiwe jamii isiyokuwa na maadili. Tukumbuke kuwa hata wakoloni waliwasaidia wamisionari kueneza Injili ili Injili ilainishe watu mioyo wanaopinga ukoloni.

**Changamoto**

Wazazi wengi tunawalaumu watoto kwa kutokuwa waadilifu, ni jambo la kawaida kusikia "Heri nisingezaa kuliko kuwa na watoto kama hawa". Mambo yafuatayo yanachangia kuharibu akili ya watoto:

1. Wazazi hawana muda wa kuwafundisha watoto Neno la Mungu ambalo ndilo chanzo cha Maarifa yote ya uadilifu na kuwa na Hekima katika jamii. Wazazi wengi wanakazania elimu ya kawaida, hiyo ni sawa, lakini elimu bila Mungu ni hatari, na ndicho tunachokiona siku hizi.
2. Ugomvi wa wazazi na maisha yasiyo na amani na upendo kati ya wazazi kunako waathiri watoto kisaikolojia hasa wanapoona mmoja anaonewa, na mwingine kuonekana katili.
3. Kukosa maadili, kumbuka chochote unachonena na kutenda mbele ya mtoto ndiyo elimu unayomfundisha. Acheni tabia ya kuwatukana, kusema uongo na tabia yakuwadanganya
4. Kukosa heshima na faragha, wazazi wengi wanalala na watoto ndipo wanaiga tabia zisizoenda na umri wao.
5. Siku hizi nyumba za kupanga zimekuwa changamoto kubwa kuharibu tabia za watoto na vijana.

**Ushauri:**

Tuwe macho, tufundishe watoto wetu majumbani, Shule za Jumapili, Kipaimara na Elimu ya Kikristo mashuleni na vyuoni katika miaka 500 ya Matengenezo ya Kanisa na hata baada ya miaka 1000 baada ya Matengenezo ya Kanisa ili kanisa letu lidumu na kukua. Tena kwa njia hii tutawalinda watoto wetu dhidi ya changamoto mbali mbali.

# HUDUMA ZA KIJAMII KKKT: Wagonjwa 400 watibiwa kansa

Hospitali ya Rufaa ya KCMC iliyopo Moshi imeanza rasmi kutoa huduma ya kutibu saratani na kuifanya iwe hospitali ya tatu baada ya Hospitali ya Taifa ya Saratani Ocean Road, Dar es Salaam na Hospitali ya Rufaa ya Bugando, Mwanza.

Mkurugenzi Mkuu wa KCMC, Dkt. Gileard Masenga, akiongea jijini Arusha hivi karibuni katika hafla fupi ya kukabidhiwa gari kwa ajili ya Kituo cha Huduma ya Saratani cha KCMC, alisema kati ya 8 Desemba 2016 na Februari 2017 kituo kimeweza kuwahudumia wagonjwa 400. Lengo la Kituo hicho ni kuwa na awamu tatu na katika awamu ya kwanza ujenzi wa majengo mawili umekamilika. Jengo moja linatumika kwa ajili ya kliniki na la pili ni kwa ajili ya kutoa matibabu ya dawa za mishipa (chemotherapy). Katika awamu ya pili pia nguvu inaelekezwa katika kujenga wodi ya kulaza wagonjwa 100 na hosteli kwa ajili ya ndugu wa wagonjwa. Alisema baada ya kuanza kutoa huduma hiyo, likajitokeza hitaji la kuwa na wodi na hosteli kwa kuwa baadhi ya wagonjwa hutoka mbali na kituo.

Alisema changamoto ni kwamba dawa za tiba ya saratani ambazo hutolewa bure ni ghali sana, hivyo anawashukuru wahisani wa KCMC kutoka Marekani ambao hutoa misaada ya dawa na kufanikisha ujenzi awamu ya kwanza. Alisema wahisani hao pia wamechangisha fedha za kununua vifaa vya kutoa tiba ya mionzi lakini changamoto iliyopo ni uhaba wa fedha za ujenzi wa jengo maalumu (radiation bunker) la kuweka mashine za kutolea tiba ya mionzi linalokisiwa kugharamu takribani sh. bilioni saba.



**Katibu Mkuu wa KKKT, Bw. Brighton Killewa (kulia), akimkabidhi Mkurugenzi Mkuu wa KCMC, Dkt. Gileard Masenga, hati ya makabidhiano ya gari lililotolewa na Kanisa kwa ajili ya huduma za saratani hospitalini hapo. Kushoto ni Mchg. Lazaro Rohho, Naibu Katibu Mkuu Misioni na Uinjilisti KKKT aliyeliweka wakfu gari hilo 13 Machi 2017 na kulia ni Bw. S. Munuo, Afisa Usafiri KCMC.** (PICHA: © 2017 KKKT/ ELIZABETH LOBULU).

# Vijana na Matengenezo ya Kanisa

**Mchg. Anza Amen Lema**

Vijana ni nguvu kubwa sana katika Kanisa la Mungu. Biblia inasema: "Fahari ya vijana ni nguvu zao," (Mit 20:29a). Vijana wana nguvu iwezayo kutumika kujenga au kuharibu. Mabadiliko makubwa sana yaliyofanyika duniani waliokuwa mstari wa mbele kuyatekeleza ni vijana.

Kijana Daudi alimshinda Goliath wakati wa ujana wake. Kijana Yusufu aliishi maisha ya ushuhuda na baadaye kuchaguliwa kuwa Waziri Mkuu wa Misri. Kijana Esta msichana mdogo alimshinda Hamani (Est. 1: 1 – 2:23).

Bwana Yesu Kristo akiwa kijana alitoa huduma mbalimbali hadi alipotufia pale msalabani kwa ajili ya ukombozi wetu. Yesu aliteswa na kufa msalabani akiwa na miaka 33.

Martin Luther alizaliwa na kukulia nchini Ujerumani na alisoma masomo ya falsafa na sheria na baadaye theologia akiwa kijana. Martin Luther akiwa kijana na mwanatheolojia aliongozwa na Mungu kufanya "Matengenezo ya Kanisa." Aliandika vitabu vingi, alitunga nyimbo kadhaa na kutafsiri Biblia katika lugha ya Kijerumani. Huduma yake imeleta mabadiliko makubwa sana katika Kanisa na ulimwengu kwa jumla.

Mafundisho mbalimbali na maandiko yake yanatumika kutuelekeza kusimama imara katika maisha ya wokovu tulioupata kwa neema.

Katekisimu Ndogo, yaani mafundisho kwa ajili ya vijana Wakristo na Katekisimu Kubwa kwa ajili ya Wachungaji ni miongoni mwa tunu hizo.

Baba wa Taifa Mwl. Julius Nyerere, aliongoza taifa akiwa kijana mdogo. Akiwa kijana wa miaka takribani 30, alikuwa mstari wa mbele kuleta maendeleo katika taifa.



**Mchg. Anza Amen Lema**

Kukua kwa taifa la Japan mara tu vita ya pili ya dunia ilipokwisha kunatokana na nguvu ya vijana.

Tukiendelea kuchunguza mchango wa vijana katika maendeleo ya ulimwengu wa sayansi na teknolojia, tunakumbuka uvumbuzi wa kisayansi wa akina Isaac Newton na Albert Einstein na katika mawasiliano Mark Zuckerberg mwanzilishi wa 'Facebook' na Steve Jobs, wa 'Apple Computers'; na pia tajiri anayesaidia maskini Billy Gates. Hawa wote wamefanya maajabu kwa kutumia uwezo wa akili na ubunifu wakiwa bado ni vijana.

Taifa na Kanisa letu limejaliwa kuwa na vijana wengi wenye vipaji mbalimbali. Ninaona orodha ndefu ya viongozi wa Kanisa la KKKT ambao wameacha matunda mema sana. Viongozi walipata watangulizi wazuri ambao waliwajengea msingi imara wa imani. Jambo hili ni la msingi sana hasa tunapokumbuka "Miaka 500 ya Matengenezo ya Kanisa." Matengenezo ya Kanisa hayajawahi kukoma; ni jambo endelevu. Na katika mada hii nakumbusha kuwa kijana aone kazi aliyoifanya kijana Martin Luther haikuwa kitendo cha mara moja kilichoishia siku moja. Historia inatuonyesha mijadala na malumbano mengi ambayo kwa ujumla wake yalileta mabadiliko ya mitazamo, mikazo, misimamo, mafafanuzi lakini hata mikakati ya jinsi ya kuendelea mbele.

Mabadiliko yoyote kwa kawaida yanaanza na kijana mmoja na kusambaa. Hata imani yetu ya kikristo ilianzishwa na Yesu mwenyewe na kusambaa dunia nzima. Ndio maana tunapoangalia idadi ya wahusika tunaona kwamba jambo ambalo lilianza kwa kijana Martin Luther kugongea "Hoja 95" katika mlango wa Kanisa lilikuja kuhusisha watu wengine jinsi siku zilivyosonga mbele. Tunaona kwamba jambo lililoanza pasipo mkakati maalum wa mpango na mwelekeo, lilifikia hatua ya kujenga mfumo wa mafundisho na hatimaye kuzaa madhehebu mengi. Martin Luther hakuwa na mpango na mwelekeo wa kuligawa Kanisa nje bali kulirejeza kanisa katika imani iliyojikita katika Neno la Mungu. (**Mchg. Anza Amen Lema ni Mratibu wa Vijana KKKT**)

# Viongozi wa KKKT na NALC wakutana Arusha

**Na Mwandishi Wetu**

Viongozi wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) na wa Kanisa la Kilutheri la Amerika ya Kaskazini (NALC) walikutana 30 Januari 2017. KKKT iliwakilishwa na Mkuu wa KKKT, Askofu Dkt. Fredrick O. Shoo aliyefuatana na Katibu Mkuu wa KKKT, Bw. Brighton Killewa.



**Kutoka kushoto ni Msaidizi wa Askofu Huduma na Ekumene wa Kanisa la NALC, Mchg. Dkt. David Wendel; Mkuu wa KKKT, Askofu Dkt. Fredrick O. Shoo; Kiongozi wa NALC, Askofu John F. Bradosky na Katibu Mkuu wa KKKT, Bw. Brighton Killewa.** (Picha: © 2017 ELCT/ E. LOBULU)

Ujumbe wa NALC ulioongozwa na Askofu John Bradosky aliyefuatana na Msaidizi wa Askofu Huduma na Ekumene katika Kanisa la NALC, Mchg. Dkt. David Wendel.

Mazungumzo yao yaliyofanyika Ofisi Kuu ya KKKT, Arusha pamoja na mambo mengine yalihusu historia ya kuanzishwa kwa NALC; Mkataba wa Mauhusiano baina ya KKKT na NALC uliotiwa saini Agosti 2013 na malengo ya msingi ya makanisa hayo mawili.

Kabla ya kuja Tanzania ujumbe wa NALC ulitembelea Kanisa la Kiinjili la Ethiopia Mekane Yesus (EECMY) ambalo lilikuwa na Mkutano Mkuu tarehe 22 – 28 Januari, 2017. Mkutano huo ulimchagua Mchg. Yonas Yigezu kuwa Rais wa Kanisa la EECMY ambaye ataongoza Kanisa hilo kwa miaka minne.

# Dayosisi kuanzisha miradi ya pamoja



**Picha ya pamoja ya viongozi wa Dayosisi na washiriki wengine toka Ukanda wa Kusini (Southern Cluster) waliohudhuria warsha mjini Morogoro hivi karibuni na kupatana kuanzisha miradi ya kiuchumi katika ukanda huo. Washiriki walitoka Dayosisi za: Kusini, Konde, Iringa, Mashariki na Pwani, Morogoro, Dodoma, Ulanga-Kilombero, Kusini Kati, Kusini Magharibi, Kusini Mashariki, Ruvuma na Ziwa Tanganyika.**

## Jipatie Mada za Mkutano wa Wachungaji UDOM

Tunafurahi kuwatangazia wasomaji wote kwamba kanda za DVD za matukio ya Mkutano wa Wachungaji wote wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), uliofanyika Chuo Kikuu cha Dodoma mwezi Septemba mwaka jana, zinapatikana Ofisi ya Hazina KKKT Makao Makuu. Wasiliana kwa sms na Bi Evelyne Kivo **0764-889-735** au Mchungaji Lazaro Rohho **0784-901-277**.




**Soma mada katika tovuti ya KKKT:**
www.elct.org/documents-downloads.htm

# Viongozi wapya: Mchg. Gaville kuwekwa wakfu Juni 2017



Askofu mteule Mchungaji Blaston Gaville (kushoto) akiwa na Msaidizi wa Askofu mteule Mchg. Himid Sagga mara baada ya Mkutano Mkuu kuwachagua kuongoza Dayosisi ya Iringa Oktoba 2016. (Picha: © 2016 KKKT DIRA/ Sadataley Blogspot)

**Na Mwandishi wetu**

Mchungaji Blaston Tuluwene Gaville atawekwa wakfu kuwa Askofu wa Pili wa Dayosisi ya Iringa tarehe 25 Juni mwaka huu.

Mkutano Mkuu wa Dayosisi ya Iringa uliofanyika 4 - 7 Oktoba 2016 Chuo Kikuu cha Iringa ulimchagua Mchg. Gaville kuwa Askofu na Mchg. Himidi John Sagga kuwa Msaidizi wa Askofu.

Mchg. Gaville atachukua nafasi iliyoachwa na Askofu Dkt. Owdenburg M. Mdegella aliyestaafu.

Kabla ya kuteuliwa kuwa Askofu, Mchg. Gaville, alikuwa Msaidizi wa Askofu Dayosisi ya Iringa; nafasi iliyochukuliwa na Mchg. Sagga.

# Askofu Nasari Meru



Mkuu wa Kanisa Askofu Dkt. Fredrick Shoo akimtambulisha kwa washarika, Askofu Elias Kitoi Nasari (mwenye fimbo) baada ya kumwingiza kazini kuwa Askofu wa Dayosisi ya Meru huku mkewe Bibi Eliashukura Elias Nasari akitabasamu.

Mnamo Januari 15 Mchg. Elias Kitoi Nassari aliwekwa wakfu kuwa Askofu wa Pili wa Dayosisi ya Meru ya Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) akifuata nyayo za Askofu Dkt. Paulo Akyoo aliyestaafu baada ya kutumika katika nafasi hiyo kwa miaka 24 tangu 1993 Dayosisi hiyo ilipozaliwa.

Askofu Nasari alizaliwa 22 Desemba 1953 Kijiji cha Mulala, Meru na alikuwa Msaidizi wa Askofu wa Dayosisi ya Meru kati ya 1992 na 2003.

Alichukua masomo ya Theolojia 1979 -1983 Chuo cha Kilutheri cha Theolojia Makumira (ambacho sasa ni Chuo Kikuu) na mnamo 8 Januari 1984 alibarikiwa kuwa Mchungaji ambaye alifanya kazi katika Sharika mbalimbali za Dayosisi ya Kaskazini na baadaye Meru.

**Soma zaidi katika tovuti ya KKKT: www.elct.org/news/2017.01.001.html**

# Askofu Sendoro Mwanga

Idadi ya Dayosisi za Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) inazidi kuongezeka baada ya Dayosisi ya baada Mwanga kuzinduliwa mwezi Novemba mwaka jana. Dayosisi hiyo ilitokana na kugawanyika kwa Dayosisi ya Pare; iko katika Wilaya ya Mwanga, Kilimanjaro.

Mkutano Mkuu wa Kwanza uliofanyika Mwanga tarehe 14 Julai 2016 uliwachagua Mchg. Chediel Elinaza Sendoro kuwa Askofu na aliyekuwa Msaidizi wa Askofu wa Dayosisi ya Pare, Mchg. Timothy Msangi, alichaguliwa kuwa Msaidizi wa Askofu Dayosisi ya Mwanga.

Mchg. Sendoro aliwekwa wakfu kuwa Askofu na kuingizwa kazini kuwa Mkuu wa Dayosisi ya Mwanga na Mchg. Timothy Msangi aliingizwa kazini kuwa Msaidizi 6 Novemba 2016.

**Soma wasifu wa viongozi hao katika tovuti ya KKKT: www.elct.org/news/2016.08.001.html**



Askofu Chediel E. Sendoro, Dayosisi ya Mwanga.

## Matengenezo ni endelevu

Makanisa ya Kimatangenezo siku kwa siku yanaendelea kutengenezwa na kuhuishwa.

Pamoja na kuanzia Wittenburg, Ujerumani, Matengenezo yameenea dunia nzima na kupeleka ushuhuda wa Injili ya Yesu Kristo japo kwa maudhui, utamaduni, tathmini au mitizamo mbalimbali kuhusiana na Kanisa.

Je Kanisa limetoa mchango au vipawa gani kwa jumuiya ya Kilutheri ambayo imetokana na kuenea kwa matengenezo? Je wengine wanawezaje kufaidika na michango au vipawa hivyo?

Katika toleo hili ukurasa wa 19 kuna makala ya "Fahamu historia ya KKKT" inavyoeleza jinsi kupanuka kwa huduma za Kanisa nchini na nchi jirani kulivyo na uhusiano na historia ya matengenezo.

## Askofu Younan apewa tuzo

Fungamano la Makanisa ya Kilutheri Duniani (FMKD) limempongeza Rais wa Fungamano hilo, Askofu Dkt. Munib Younan kwa kuteuliwa kupokea tuzo ya amani ijulikanayo kama ***"Niwano Peace Prize."***

Tuzo hiyo imetokana na jitihada zake za kuongoza mazungumzo na madhehebu mbalimbali ya Kikristo na kati ya wakristo na watu wa dini nyingine kama Waislamu na Wayahudi waliopo Jerusalemu na duniani kote.

Dkt. Younan ni Askofu wa Kanisa la Kilutheri Jordan na Nchi Takatifu. Mkutano Mkuu wa 11 wa FMKD uliofanyika Stuttgart, Ujerumani mwaka 2010 ulimchagua kuwa Rais wa FMKD kwa miaka saba.



**Askofu Dkt. Munib Younan, Rais wa Fungamano la Makanisa ya Kilutheri Duniani.**

Katibu Mkuu wa FMKD, Mchg. Dkt. Martin Junge, alimpongeza Askofu Dkt. Younan na kusema hivi karibuni kwamba tuzo hiyo imethibitisha kwamba amani ni jambo muhimu linalowezekana. Dkt. Junge ametaka "tusiondoke katika njia inayotuelekeza kujenga amani katika dunia iliyojaa machafuko na mateso."

(CHANZO: LWI)

# Matengenezo na kutunza uumbaji

**Tumeitiwa na Mungu kuwa marafiki na mawakili wema wa uumbaji.**

**Na Mchg. Mexon Mung'ong'o**

Mara kwa mara tunaona habari kuhusu uharibifu wa mazingira katika vyombo vya habari. Aidha, vyombo hivyo vinaonyesha taarifa za ujangili dhidi ya viumbe mbalimbali kama tembo, vifaru, sokwe, pundamilia nk.

Kanisa na jamii wameshuhudia mazingira yakiharibiwa kupitia shughuli za kilimo, uchimbaji wa madini, uvuvi na uwindaji haramu na uharibifu wa misitu, ujenzi wa miundombinu mbalimbali ili kurahisisha na kuboresha maisha. Uongezekaji wa viwanda na matumizi ya vyombo vya moto vinavyotumia mafuta navyo hutoa moshi wa sumu inayoharibu angahewa, ardhi na viumbe.

Matokeo ya uharibifu huo umechangia mabadiliko ya tabianchi, kwa kuongezeka joto duniani, upungufu wa mvua na hata majira ya mvua hubadilika badilika, nk.

Uchungu wa madhara ya uharibifu wa mazingira unagusa viumbe vyote (Rum 8: 19 - 23). Mfano, maji au mvua vinapokosekana viumbe vyote huugua kuelekea kifo, maana hakuna kiumbe hai kiwezacho kuishi pasipo maji. Aidha, angahewa linapochafuliwa kwa sumu, viumbe hai vinapovuta hewa hiyo, vinaugua magonjwa hatari ya kufisha.

Shirika la Afya Duniani linakadiria kwamba watu milioni 2.4 hufa kila mwaka duniani kwa magonjwa yanayohusiana na mfumo hewa. Magonjwa na vifo husababisha uchumi wa mtu mmoja mmoja hata taifa kuathirika kwa ajili ya kuuguza, matibabu na mazishi. Aidha, vifo husababisha kutokea kwa yatima, wajane na wagane wengi.

KKKT inapoungana na Walutheri wengine duniani kuadhimisha "Miaka 500 ya Matengenezo ya Kanisa", inahitaji kujihoji pia juu ya utume wake dhidi ya uharibifu wa mazingira/ uumbaji wa Mungu. Walutheri hukiri 'Imani ya Kikristo' katika Ibada. Sehemu ya kwanza inasema: "Namwamini Mungu, Baba Mwenyezi, Muumba wa mbingu na nchi."

Ukisoma "Katekisimo Ndogo ya Martin Luther na Maelezo Yake" ukurasa wa 127, utakutana na swali nambari 112 lisemalo: 'Twamwia nini Baba yetu wa mbinguni kwa wema wake wote?' Swali linajibiwa kuwa, wajibu wetu ni:
(a) Kumshukuru na kumsifu, kumtumikia na kumtii. (b) Kuwa mawakili wema wa uumbaji wake (Mwa 2:15). Kisha limewekwa angalizo kuwa, "Tu mawakili wema tunapoepuka kuchafua hewa, nchi na maji; tukitupa takataka vizuri; tukitumia kuliko kuharibu rasilimali; kutunza kuliko kuharibu nguvu au nishati; kuendeleza vitu au kuvitumia tena kila inapowezekana; na kuthaminisha na kutunza uumbaji wote wa Mungu."

Kutokana na 'Ukiri wa Kikristo', Walutheri na jamii yote tumeitiwa kuwa marafiki na mawakili wema wa uumbaji. Aidha, mazingira yanayotunzwa ndiyo yanayotuzawadia "alama za nje zinazoonekana" ambazo hutumika kwenye Sakramenti ya Ubatizo na Meza ya Bwana. Sakramenti kwa Mlutheri ni chombo cha neema ya Mungu kwa ajili yetu. 'Alama za nje zinazoonekana' ni maji kwa ajili ya Ubatizo; Mkate (ngano) na mvinyo (zabibu) kwa ajili ya Meza ya Bwana. Hivyo, kila tunapoadhimisha Sakramenti hizo, tunazawadiwa neema ya Mungu, lakini ni wakati ule ule tunakumbushwa kuthamini na kuyatunza mazingira yaendelee kutuzalishia "alama za nje" za Sakramenti.

Wito kwa Kanisa ni kuendelea kuamsha mioyo ya wakristo na jamii kuyapenda, kuyathamini na kuyatunza mazingira kama Mungu afanyavyo kwa uumbaji wake wote (Zab. 104:10-31).

Uwepo wa Kitengo cha Uhai na Mazingira Makao Makuu ya KKKT, kuchochee Dayosisi zote kuwa na Kitengo cha aina hiyo kwa ngazi zote hadi jumuiya. Aidha, vyuo vya Kanisa letu vihamasishwe kuwa na mitaala inayoingiza masomo ya mazingira/ uumbaji kwa mtazamo wa Ki-Biblia.

Mungu atujalie neema sisi sote tuliokutana na mada hii, kufanyia matengenezo fikra na nafsi zetu. Tujue kuwa kutunza mazingira ni sehemu ya Imani yetu ya Kikristo. Hivyo, 'tutunze mazingira ili maisha yaendelee kwa kizazi cha sasa na cha baadaye.' Amen.

# Watumishi Ofisi Kuu ya KKKT waadhimisha SIKU YA MAOMBI YA DUNIA 2017





**Kauli mbiu ya 2017:** Je sijatenda iliyo haki kwako? (Mt 20: 1 - 16).





# Watunukiwa zawadi kwa kutunza mazingira

Mratibu wa Kitengo cha Uhai na Mazingira KKKT, Bibi Patricia Mwaikenda Mchome, alisema hivi karibuni kwamba ni mwaka wa tano tangu Kanisa liwe na juma la mazingira ambayo ni juma la tatu mwezi Machi. Lengo la juma hilo ni kuhamasisha washarika na watu wote kupanda miti na kuzuia uharibifu wa mazingira. Alisema: "Utunzaji wa Mazingira ni agizo la Mungu tangu alipomwagiza Adam alime na kuitunza bustani." Asema kila mmoja anawajibika kuendeleza uhai kwa kuacha kukata miti ovyo na badala yake kupanda miti ya aina mbalimbali kama ya matunda. "Kupanda miti hakutegemei ukubwa wa eneo bali ni kuhamasika," alieleza na kutoa mfano wa watumishi waliopanda miti katika maeneo madogo na wengine wanamwagilia maji kwa teknolojia ya matone kwa kutumia chupa za plastiki.



Kutoka kulia Naibu Katibu Mkuu Mipango na Maendeleo KKKT, Bw. Mallumbo William Mallumbo, akiwa na watumishi wa Ofisi Kuu ya KKKT waliokuwa washindi kwa kupanda miti katika juma la mazingira mwaka jana. Washindi hao ni Bibi Julieth Sinare, Sista Anna Mahenge, Bw. Elinokoa Macha na Bibi Elizabeth Lobulu (hayuko pichani). Kushoto ni Bibi Patricia Mwaikenda Mchome, Mratibu wa Uhai na Mazingira KKKT, aliyeandaa hafla hiyo.

# Kikulacho ki-nguoni mwako

**Na Mchungaji Emeline Ndossi,**
**Dayosisi ya Kaskazini.**

**USEMI WA KISWAHILI**

"Kikulacho ki nguoni mwako," ni usemi wa kweli ikizingatiwa kuwa adui mkubwa wa haki za wanawake kurithi ama kusimamia mirathi ni familia zao. Katika familia nyingi baba akifariki wana familia wamekuwa vinara wa kukwamisha wanawake kupata haki zao za mirathi.

Mama mmoja alisikika akilia kwa uchungu: "Mungu wangu siamini." Ni kwa kuwa kaka yake alikiri kwamba atachukua kwa nguvu sehemu ya ardhi aliyokuwa amepewa na baba yao. Mama huyu hakutegemea kaka yake angeweza kupanga kumdhulumu mali yake.

Mama mwingine mjane alikiri "mume akifa mjane hupigwa kama kengele." Wajane wengi hugutushwa na tabia ya ndugu za mume wasio na huruma na maisha yao wanapogeuka kuwa waporaji wa mali. Baadhi ya watoto wa kike na wajane wamejikuta wakipigwa butwaa wanapokutana na nyanyaso kwani hawakutegemea ama kujiandaa kuwaona kaka zao, watoto wao waliowazaa, na ndugu za waume wakiwageuka ghafla na kuwa maadui kwa sababu ya mali.

Ndani ya familia za wazazi wao ama walikoolewa ndipo wanawake wanapopata uonevu na dhuluma kubwa zaidi kuliko katika taasisi nyingine zozote. Maana yake, 'kiwalacho kimo nguoni mwao'.

Dhuluma kutoka watu wasiowatarajia imewaacha wanawake wengi katika uchungu, mahangaiko na umaskini. Ipo tafsiri katika mila na desturi zetu kuwa ni aibu familia kuwa na mitafaruku ama kupeleka ndugu mahakamani. Kwa sababu hiyo, maonevu na dhuluma ndani ya familia nyingi hufichwa na wanawake ili kulinda heshima ya familia kwa jamii inayowazunguka.

Kuthibitisha matazamio ya jamii napenda kunukuu maneno ya hakimu mmoja aliyesema: "Mimi nashangaa sana ninapoona, mtoto anamleta baba yake mahakamani ama mke anamleta mumewe mahakamani, mimi huwa naawambia waende nyumbani wakayamalize mashauri huko." Swali la kujiuliza ni je, wanawake wanaodhulumiwa haki yao ya mirathi watamalizaje mashauri yao nyumbani iwapo viongozi wa baadhi ya familia na koo ni watu wasio na uongozi wenye uadilifu kulinda haki za wanawake?

Maoni ya hakimu ni kwa kuamini kuwa familia zote ni mahali salama kwa wanafamilia wote. Kumbe kinyume na matazamio haya sivyo ilivyo hasa kuhusiana na suala la mirathi. Nimenukuu mifano ya visa halisi kuonesha mazingira na upana wa tatizo.

**KISA CHA KWANZA**

Mama mmoja Mkristo aliishi na mumewe na kuzaa watoto wa kike watano na wa mmoja wa kiume. Mume alipofariki, mama huyu aliniambia amejikuta kwenye mgogoro mkubwa na watoto wake kwa sababu ya mali za marehemu mume wake. Yule mtoto pekee wa wakiume alidai kuwa ana haki ya kuchua mali yote ya baba yake na kwamba mama yake hana sauti juu yake. Yule mtoto alijitangaza ndiye msemaji wa mwisho wa mali ya baba yake na kwamba mama afuate anachotaka yeye.

Ni bahati mbaya kinyume na matakwa ya mama yake kuwa mwanae wa kiume huyo hataki dada zake kupata chochote toka mali ya baba yao. Hata mali ambazo mama angetaka kurithisha binti zake mvulana huyo amekataa. Madai ni kuwa yeye ndiye aliyebaki pale nyumbani atakayeendeleza ukoo. Alidai kuwa wasichana wameolewa katika familia nyingine hivyo huko waliko ndiko na haki zao za kurithi maili ziliko. Mirathi imekuwa kiini macho kuandikwa ndani ya familia kwa sababu ya ubabe na ugomvi uliopo kati ya kaka huyo na dada yake. Mama amekatwa kauli. Na jamii ama ukoo hauna pa kupita, mgogoro unapokuwa ni wa mjane na watoto wake aliowazaa.

Nadharia ya wanandugu kupelekana mahakamini nayo ni changamoto kwa kuwa ni jamii inaamini kwamba ni aibu kutatua mgogoro wa aina hii mahakamani.

Mama mjane anashangaa jinsi amebanwa na mtoto wake hana sauti na kushindwa kutimiza madai toka watoto wake wa kike kupata haki yo mirathi toka mali ya baba yao. Hii inathibitisha ukweli wa usemi usemao kuwa kimlacho mjane huyu ki nguoni mwake.

**KISA CHA PILI**

Kisa cha pili kinahusu familia iliyokuwa na watoto sita wa kiume na mtoto mmoja wa kike. Watoto wote wa kiume wameoa isipokuwa yule wa kike hakuolewa lakini amezaa mtoto akiwa bado anaishi na wazazi wake. Mtoto huyo wa kike alisema baba wa familia hiyo pasipo kumhusisha mama yao aligawa mali zote za familia pasipo kumpa kitu chochote. Kimila nyumba ya familia hurithiwa na mtoto wa kiume wa familia. Baada ya wazazi kufariki hatima ya msichana huyu na mtoto wake ipo njia panda maana hana haki ya kurithi nyumba wala urithi alioachiwa na mama yake. Kilacho maisha ya dada huyu kimo nguoni mwake.

**TAFAKARI YA VISA: WANAWAKE KUKOSA HAKI YA KURITHI**

Katika mfano wa kwanza tunaona mvulana mmoja ndani ya familia anaona ana haki ya sauti na mali ya baba yake kuliko dada zake watano. Ndivyo ilivyo pia katika kisa cha pili baba wa familia anatoa haki kwa watoto wake wa kiume watano anaacha kumpa haki mtoto wake mmoja wa kike. 'Kinachowala' wanawake wengi katika suala la mirathi ni familia zao. Hawaoni sababu ya wanawake kupata haki. Katika familia kisingizio ni kuwa watoto wa kike wanaolewa; na hata wakati mwingine wasipoolewa hali ni ile ile. Sheria kuhusu urithi zinaonesha umuhimu wa kulinda haki ya marehemu ambazo ni pamoja na wale waliokuwa wanamtegemea. Sheria nchini Tanzania hazibagui watoto wa kike na wa kiume. Zipo familia ambazo pasipo kushurutishwa na sheria hutoa haki kwa watoto wa kiume na wa kike ya kurithi mali za wazazi wao waliofariki.

**WAJANE KUNYIMWA SAUTI NA HAKI**

Tunaona katika mfano wa kwanza mvulana pekee haoni sababu ya dada zake kutoa maoni ama kumsikiliza mama yake kuhusu jinsi mali ya marehemu baba yake itakavyogawanywa. Anatoa kauli ya mwisho juu ya mirathi kuliko mama yake na wakati mwingine hata ndugu wa kiume wa marehemu jamii imeruhusu wawe na kauli juu ya mali za mumewe kuliko mjane aliyeachwa. Vivyo hivyo katika familia ya pili haki ya kugawa mali ni ya baba. Na mama na watoto hawana haki ya maamuzi. Mama aliyehusika katika kuzalisha wakati mwingine hausishwi.

Mtazamo wa kijana ndani ya kisa cha kwanza kuwa asiwape dada zake haki maana haki yao ipo kwa waume zao si wa kweli. Tunaona yanayotokea katika familia ya pili, kuwa mwanamke hana sauti juu ya mali alizozalisha na mumewe.

Hatimaye baba anagawa mali na kutompa mtoto wake pekee wa kike kama inavyoonekana katika mfano wa pili kinyume na matakwa ya mama yake na mtoto huyo. Tatizo la kutokuwa na sauti juu ya mali ya familia ni la akinamama na wasichana ndani ya familia. Dhuluma ni wazi ndani ya familia hizi na ukimya ndio tatizo kubwa zaidi kwenye familia zinazowanyima wanawake haki ya mirathi. Mambo yanayosababisha ukimya katika familia hizi ni pamoja na baadhi ya wajane na hata wasichana kukubali kuwa ni sawa wao kutorithi chochote toka familia zao. Japo hakuna mtoto ambaye asigependa kupata urithi toka kwa wazazi wake; lakini wanawake wengine wanazidiwa nguvu na watoto wao wa kiume na wanaukoo wenye mawazo kandamizi. Inawezekana wanawake wengi wanafungwa vinywa kutokana na mila na desturi za jamiii kwamba kwenda mahakamani ni kudhalilisha familia na ndugu. Wapo wengi wasiojua la kufanya wanapokutana na ukatili wa kijinsia wa kudhulumiwa haki zao za mirathi. Na wengi hawamudu gharama za mahakama ili kujitetea na kudai haki yao.

**JUMLISHO**

Ni kweli kuwa 'kinachowala wanawake wengi ki nguoni mwao' kwa maana kuwa ni familia zile zile zinazotakiwa kuwatunza, kuwalinda na kuwapa haki yao ya mirathi wakati mwingine ndizo zimekuwa vinara katika kuwakandamiza nakuchukua haki zao.

**Wasiliana na Mchungaji Emeline Ndosi kwa sms: 0768 357 409**

# FAHAMU HISTORIA FUPI YA KKKT

## Vyama vilivyoeneza Ulutheri

Mwanzo wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanganyika (baadaye Tanzania) kuwepo nchini ni mwaka 1887, Chama cha Misioni cha 'Berlin III' au 'Evangelical Missionary Society for East Africa' (EMS) kutoka Ujerumani kilipoanzisha kazi ya Injili Kigamboni, Dar es Salaam.

## Chama cha pili

Chama cha Misioni cha 'Berlin I', nacho kutoka Ujerumani, kiliingia Tanzania kikitokea Afrika ya Kusini na kuanza kazi Nyanda za Juu Kusini mwaka 1891 kilipoanzisha kituo au misheni sehemu iitwayo Ipagika au Pipagika (Wangemannshöhe) katika Dayosisi ya Konde (kwa sasa).

Mwaka 1890 Chama cha Berlin III kilichukua sura mpya baada ya kubadili sera yake na kujulikana kwa jina la Bethel au Misioni ya 'Bethel'. Misioni hii ikafika sehemu za Tanga na kuanza kazi eneo la Mbuyukenda.

Baadaye Misioni hii iliamua kufikisha Injili ya Kristo nje ya mipaka ya Tanganyika. Wamisionari hao walipanga kwenda Rwanda kupitia Bukoba. Walipofika Bukoba wakafungua kituo mwaka 1910.

## Chama cha Leipzig

Chama cha tatu kufika nchini Tanzania ni Chama cha Misioni cha Leipzig, nacho kutoka Ujerumani. Kiliingia nchini Tanzania mwaka 1893 na kuanza kazi ya misioni Kaskazini mwa nchi sehemu ya Kidia, Old Moshi na baada ya muda mfupi, kwa kushauriwa na Mtawala wa Kijerumani, Carl Peters, wakahamia Nkwarungo - Machame.

Pamoja na vyama vilivyoanzisha Ulutheri Tanzania, kuna mchango mkubwa wa vyama vya misioni na makanisa toka Ulaya na Marekani tunayo endelea kushirikiana nayo kama: COS, ELCB, FELM, DLM, DANMISSION, SEM, LMW, MEW, NLM, NMZ, BMW, UEM, VELKD, ELCA, nk. Hakika Neno la Mungu linaendelea kufundishwa kwa upendo na kwa usahihi wakati wote huu.

## Vita za Dunia

Kanisa la Kilutheri nchini lilipita katika nyakati ngumu vipindi vya Vita Kuu ya Kwanza ya Dunia 1914 - 1918 na ya Pili 1939 - 1945. Chama cha Misioni Augustana kutoka Marekani pamoja na Walutheri kutoka nchi nyingine za Ulaya walitoa msaada sana wakati wamisionari wa Kijerumani walipoondoka.

## Makanisa Saba

Vyama vya misioni viliendelea na kazi ya Injili na makanisa saba ya Kilutheri yakaanzishwa maeneo mbalimbali nchini. Makanisa hayo mwaka 1948 yaliunda Fungamano la Makanisa ya Kilutheri Tanganyika. Na tarehe 19 Juni 1963 makanisa yale saba yaliungana kuunda Kanisa moja la **KKKT** na makanisa yakageuka kuwa Dayosisi/ Sinodi. Sinodi zikageuka kuwa Dayosisi na tangu Novemba 2016 KKKT ina Dayosisi 25.

## Uongozi na usimamizi

Chombo kikuu cha maamuzi KKKT ni Mkutano Mkuu ambao hufanyika kila baada ya miaka minne. Halmashauri Kuu ya KKKT hukutana mara mbili kwa mwaka kwa vikao vyake vya kawaida. Wajumbe wa vyombo vyote hivi wanawakilisha Dayosisi zote za KKKT.

## Kazi za Umoja

Kanisa lina vituo na Ofisi Kuu ya Kazi za Umoja (Common Work). Ofisi Kuu ya Kanisa inaongozwa na Katibu Mkuu. Ina idara zifuatazo: Misioni na Uinjilisti; Mipango na Maendeleo; Fedha na Utawala; Huduma za Jamii, Kazi za Wanawake na Watoto. Pia kuna Kitengo cha Ukaguzi. Kazi ya Ofisi Kuu ya KKKT ni pamoja na ***kuratibisha, kuwezesha na kufanya utetezi*** kwa manufaa ya Kanisa zima.

KKKT ina taasisi na vituo vinavyotunza Kazi za Umoja: **1.** Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira **2.** Seminari Ndogo ya Kilutheri Morogoro **3.** Kituo cha Redio Sauti ya Injili, Moshi. **4.** Shule za Msingi kwa watoto viziwi Mwanga na Njombe. **5.** Shule ya Sekondari kwa watoto viziwi Njombe. **6.** Miradi ya kuongeza kipato.

Pamoja na vituo vya Kazi za Umoja, Dayosisi zina hospitali 23 na zahanati / vituo vya afya 150. Dayosisi zote zina shule za msingi, sekondari na vyuo vya ufundi na maarifa mbalimbali. Baadhi ya Dayosisi zina vyuo vikuu. Taasisi hizi hutoa huduma kwa watu wote bila ubaguzi.



**Mkuu wa KKKT,**
**Askofu Dkt. Fredrick Onael Shoo.**

Karibu kila dayosisi /taasisi zake/ idara zina miradi midogo midogo ya kuinua kipato; miradi ya maji salama, miradi ya ng'ombe wa maziwa, nk. Dayosisi nyingi zina miradi mikubwa na ya kati. Baadhi zimeanzisha mabenki au vyama vikubwa vya kuweka na kukopa (SACCOs).

## Kazi za Misioni

KKKT inajihusisha na kazi za misioni ndani na nje ya Tanzania. Baadhi ya maeneo nje ya nchi ni Jamhuri ya Demokrasia ya Kongo, Msumbiji, Malawi, Uganda na Zambia. Ndani ya nchi maeneo ya misioni ni Tabora, Kigoma na Zanzibar.

## Ushirikiano na wengine

KKKT ni mwanachama hai wa: Jumuiya ya Kikristo Tanzania (CCT); 'Lutheran Mission Cooperation' (LMC); Baraza la Makanisa Barani Afrika (AACC); Fungamano la Makanisa ya Kilutheri Duniani (LWF) na Baraza la Makanisa Duniani (WCC).

## Ofisi zilipo

Ofisi Kuu ya KKKT ipo Arusha "Lutheran Centre", Barabara ya Boma mkabala na Posta Kuu. Senta hiyo ina hosteli kwa ajili ya watumishi wa Kanisa.


**Kwa maelezo zaidi wasiliana na**

**Katibu Mkuu**

Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania

**S.L.P.** 3033, **Arusha**

**Simu: 250 8856/ 250 8857**

**Fax** 254 8858

**Barua pepe:** elcthq@elct.or.tz

**Tovuti: http//**www.elct.org/

**Au: http//**www.elct.or.tz/



Moshi Lutheran
Printing Press
Tunachapisha:
Vitabu vya aina zote
Majarida na Magazeti
Hati za Fedha
Madaftari
Bahasha
Vipeperushi
Tiketi za vyombo vya Usafiri
Mabango ya matangazo
kadi za Kila aina
Pia tunatoa huduma za:
Type Setting na Usanifu
Ukarabati vitabu Chakavu
Wasiliana nasi:
Moshi Lutheran Printing Press
S.L.P 301, Moshi
Kilimanjaro
Simu: +255 272 750 546
Mob: +255 752 327 89